# MAJARIBIO YA MTIHANI DARASA LA TANO

# MUHULA WA KWANZA-KISWAHILI-2019

*1. Hakikisha umeandika*
*(i)Jina lako (ii)Jina la shule yako*

***Muda: Saa 1 Dak. 40***

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15 . Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Alipoitwa na babake __1__ yaliyokuwa yametokea __2__ mzazi huyu hakujishughulisha sana na mambo __3__. Walisema __4__ chache sana alipokuwa __5__ amnunulie chochote alichotaka. Hakujua kama ni hali ya __6__ au pengine baba yake hakupenda kusema sana tu. Kila __7__ nyumbani alimwalimu __8__ mahali pale pale maalum akaanza kutazama runinga. Naye alikuwa na kiti chake pembeni __9__ mezani akifanya kazi __10__ ya ziada. Mama yake alijishughulisha na upishi __11__ ulimfurahisha sana. Nyumba hii __12__ daima imetulia na wenyeji __13__ kelele. Alifikiri tabia hii __14__ iliyochangia utulivu wake mkuu hata darasani __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. alifahamu | B. hakujua | C. hakujuwa | D. alielewa |
| **2.** | A. kwani | B. pia | C. ili | D. kuwa ni |
| **3.** | A. zake | B. chake | C. lake | D. yake |
| **4.** | A. nyakati | B. wiki | C. wasaa | D. saa |
| **5.** | A. anamtaka | B. alichomtaka | C. akimtaka | D. aliomtaka |
| **6.** | A. kuumba | B. kuumbika | C. kimaumbile | D. maumbo |
| **7.** | A. hajaingia | B. aliingia | C. alipoingia | D. akitaka kuingia |
| **8.** | A. akaketi | B. ameketi | C. angaliketi | D. aliketi |
| **9.** | A. alipokaa | B. alishauri | C. aliona | D. alisimama |
| **10.** | A. zake | B. yake | C. lake | D. wake |
| **11.** | A. ambacho | B. ambalo | C. ambao | D. ambayo |
| **12.** | A. ilikuwa | B. ilikua | C. ilikuua | D. ilikuaa |
| **13.** | A. wafanya | B. hawakupenda | C. walithamini | D. hawakuchukia |
| **14.** | A. ndiyo | B. ndilo | C. ndicho | D. ndio |
| **15.** | A. lao | B. pao | C. yake | D. yao |

Compiled and supplied by Schools Net Kenya P.O. Box 15509-00503. Nairobi-Tel:+254202319748 |
E-Mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

**Kutoka swali 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.**

16. **Kamilisha methali:-**

    Mkono mtupu

    A. haulambwi B. haulabwi
    C. haurambwi D. hautajwi

17. **Tumia o-ote kukamilisha sentensi:-**

    Kipepeo __________ anapendeza.

    A. chochote B. wowote
    C. yeyote D. lolote

18. Juma alinunua mkate. Aligawana na wenzake watatu sawa sawa. Kila mmoja alikula ______.

    A. robo B. thuluthi
    C. tusui D. khumusi

19. Mtoto wa ng'ombe ni ndama kama vile mtoto wa ndege ni __________.

    A. kitungule B. shibli
    C. kinda D. kifaranga

20. Mkonge ni mmea wenye ___________ mikali.

    A. mimba B. miiba
    C. matawi D. mizizi

21. Seremala hutumia nini kulainisha mbao?

    A. Msumeno B. Msasa
    C. Nyundo D. Randa

22. **Kitendawili:-**

    Popo mbili zavuka mto.

    A. Macho B. Daraja
    C. Maji D. Miguu

23. **Kanusha:-**

    Mwalimu amekuja leo.

    A. Mwalimu hajaja leo.
    B. Mwalimu hatakuja leo.
    C. Mwalimu haji leo.
    D. Mwalimu hajaja jana.

24. Chagua sentensi sahihi.

    A. Karatasi hizi ilipotea ni yangu.
    B. Darasa lililofagiliwa ni langu.
    C. Ukucha ambayo ina uchafu ni hii.
    D. Kiroboto ambacho kilivuka kimepotea.

25. Kinyume cha kusini ni __________.

    A. Kaskazini
    B. Mashariki
    C. Magharibi
    D. Kaskazini Magharibi

26. **Andika wingi:-**

    Sijakuona ukiwa huna kofia.

    A. Sijawaona ukiwa hana kofia.
    B. Sijawaona mkiwa hamna kofia.
    C. Sijawaona mukiwa mna kofia.
    D. Sijawaona mkiwa mna makofia.

27. Mwalimu wetu ana __________ __________.

    A. ndefu/defu B. ndefu/ndevu
    C. ndevu/defu D. ndevu/ndefu

28. Kazi ifaayo buli ni __________.

    A. kuwekea chai B. kuokea mikate
    C. kuchemshia chai D. kupepeta ngano

29. **Andika kwa tarakimu:-**

    Elfu ishirini na mbili mia mbili na mbili.

    A. 22202 B. 20222
    C. 2200 D. 22022

30. Vazi lililounganishwa shati na suruali na huvaliwa juu ya nguo za kawaida ili kuzuia zisichafuke wakati wa kufanya kazi linaitwa?

    A. Shimizi B. Joho
    C. Surupwenye D. Kanzu



Compiled and supplied by Schools Net Kenya P.O. Box 15509-00503. Nairobi-Tel:+254202319748 |
E-Mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 31 - 40.**

Imani na Amani ni watoto watukutu. Siku moja walitoroka kwao na kujificha shambani. Mjomba wao alipowaona walikimbia wakaingia msituni. Walipofika katikati ya msitu waliona mti wenye matunda mazuri. Matunda hayo yalifanana na machungwa. Walikwenda mpaka chini ya mti ule. Mti huo ulikuwa mtonga.

Walipofika hapo, walianza kuchuma matunda. Mara walimwona nyoka mkubwa. Amani na Imani walianza kukimbia. Walikimbia wakakimbia, na wakakimbia. Hapo walianza kujuta kwa nini walitoroka nyumbani walipofika nyumbani walifokewa sana walikuwa wakihema sana hata kwa muda hawangeongea. Baadaye walitubu na kusamehewa.

**31.** Neno watukutu lina maana gani kulingana na taarifa hii?

A. Watiifu B. Wakaidi
C. Waaminifu D. Wasikivu

**32.** Kwa nini watoto walijificha?

A. Kuwatoroka wazazi
B. Kwenda kula matunda
C. Kumtoroka mjombao
D. Hatujaelezwa

**33.** Unafikiri watoto hawa walihitaji adhabu?

A. Ndio
B. Haiwezekani
C. La
D. Haijulikani

**34.** Matunda ya mtonga yanaweza kuitwa ______.

A. maembe B. ndizi
C. papai D. tonga

**35.** Kati ya hawa ni nani aliyeogopwa na watoto?

A. Baba B. Kaka
C. Mjomba D. Mama

**36.** Kuchuma ni kutoa matunda mtoni ilhali kuchuna ni __________.

A. kutoa ngozi B. kumwaga maji
C. kutoa mboga mtini D. kukwea mti

**37.** Pale mtini palikuwa na _________.

A. mjomba B. joka
C. nyuni D. majani

**38.** Ni neno gani lenye maana sawa na msituni?

A. Kichaka B. Miti
C. Pori D. Mbuga

**39.** Methali gani inafaa kuelezwa watoto kama Amani na Imani?

A. Haraka haraka haina baraka
B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
C. Mbio za sakafuni huishia ukingoni
D. Pole pole ndio mwendo

**40.** Watoto walisamehewa baada ya _________.

A. Kumaliza kula matunda
B. Kutokiri makosa yao
C. Kukiri makosa na kuomba msamaha
D. Kutoroka nyumbani na kuhema



Compiled and supplied by Schools Net Kenya P.O. Box 15509-00503. Nairobi-Tel:+254202319748 |
E-Mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 41 - 50.**

Nchi yetu ya Kenya inasifika kote duniani kutokana na hali nzuri ya hewa. Nchi yetu hupatikana katika eneo la ikweta. Jua hupatikana kwa mwaka mzima. Hali hii nzuri ya hewa ndiyo huwavutia watalii chungu nzima kutoka kila pembe ya dunia kama vile Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na hata Ujapani. Utawapata pia watalii ambao huja nchini ili kupanda mlima Kenya ambao juu yake huwa na baridi kali sana, baridi hii hugandamana na kuwa barafu na pale kileleni cha mlima Kenya kuna theluji ambayo huwa nyeupe.

Ukiteremka na kuelekea mwambao wa pwani viwango vya joto huwa juu kutokana na bahari Hindi. Maeneo ya ziwa Victoria pia hupata viwango vya juu vya joto. Kuna pia mbuga na hifadhi za wanyama. Hili huwa ni vutio kubwa kwa watalii ambako kuna wanyama kama simba, tembo, nyati, chui na duma ambao ndio wanyama watano wakuu miongoni mwa wengine wengi.

Nchini pia kunayo mianguko ya maji ya Thompson, Chania na Fourteen Falls. Sehemu hizi huwavutia watalii wa humu nchini na pia wengi kutoka ng'ambo. Tunamshukuru Mola kwa kutupatia nchi nzuri yenye sifa teletele.

41. Nchi yetu ya Kenya inasifika kote duniani kwa ajili ya ________.
A. watu wake
B. baridi yake
C. hali mzuri ya hewa
D. hali duni ya hewa

42. Nchi yetu hupatikana katika eneo la _______.
A. kati
B. chini
C. mbali
D. ikweta

43. Jua hupatikana nchi nzima kwa muda wa _____.
A. siku chache
B. miezi sita
C. miaka miwili
D. mwaka mzima

44. Watalii wanaokuja nchi yetu ni chungu nzima, hivi ni kusema kuwa ni ___________.
A. kadhaa
B. wachache
C. si wengi
D. wengi

45. Watalii wanaokuja Kenya waliotajwa ni wote hawa isipokuwa?
A. Wajerumani
B. Wagiriki
C. Wafaransa
D. Wajapani

46. Juu ya milima kama mlima Kenya huwa kuna ___________.
A. baridi kiasi
B. joto sana
C. theluji
D. rangi nyeupe

47. Nchini Kenya ukielekea upande wa mwambao wa pwani ___________.
A. baridi hupunguka
B. jua huangaza sana
C. huwa na viwango vya juu vya joto
D. huwa na viwango vya chini vya joto

48. Mbuga na hifadhi za wanyama pia huwa _____.
A. si mahali panapopendeza
B. vutio kubwa kwa watalii
C. vutio kubwa la wanyama
D. vutio kubwa kwa wanasiasa

49. Chania, Fourteen falls na Thompson ni _____.
A. mito
B. ziwa
C. chemchemi
D. mianguko

50. Habari hii ni kuhusu __________.
A. Utalii wetu
B. Nchi yetu
C. Milima na wanyama wetu
D. Mbuga na hifadhi zetu



Compiled and supplied by Schools Net Kenya P.O. Box 15509-00503. Nairobi-Tel:+254202319748 |
E-Mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com